



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUSITISHA HUDUMA KWA WANACHAMA WA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF) KATIKA HOSPITALI ZA AGA KHAN

Dodoma, Agosti 11, 2024

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unakiri kupokea maombi ya Hospitali ya Aga Khan ya kusitisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wanachama wa NHIF kutokana na sababu za kiundeshaji za hospitali hiyo ifikapo Agosti 13, 2024. Kwa mujibu wa Mkataba baina ya Mfuko na Mtoa Huduma, upande wowote unayo haki ya kuomba kusitisha au kuendelea na utoaji wa huduma, hivyo Aga Khan kama ilivyo kwa vituo vingine anao uhuru wa kutumia haki ya kimkataba.

Wakati majadiliano na Mtoa Huduma yakiendelea kuhusu maombi yake ya kusitisha huduma, Mfuko unatoa taarifa kwa wadau wake wote kuwa, ifikapo tarehe tajwa hapo juu, wanachama wanashauriwa kutumia vituo mbadala vilivyosajiliwa na Mfuko kupata huduma za matibabu.

Mfuko umesajili vituo zaidi ya 9000 nchini ambavyo vinamilikiwa na Serikali, Taasisi Binafsi na Mashirika ya Dini. Vituo hivi ni vya ngazi mbalimbali kuanzia Zahanati hadi ngazi ya Hospitali ya Taifa ya Rufaa. Lengo la kusajili vituo hivyo ni kumpa uhuru mwanachama kuchagua kituo cha kupata huduma za matibabu popote alipo ndani ya nchi.

Mfuko umefanya maandalizi ya kuwezesha mwendelezo wa huduma kwa wanachama waliokuwa wanapata huduma katika hospitali ya Aga Khan ikiwemo kusajili vituo mbadala vyenye hadhi sawa au zaidi ya Hospitali hiyo. Aidha, Ofisi za NHIF nchini pamoja na Kituo cha Mfuko cha Huduma kwa Wateja zimejipanga kuhakikisha wanachama hawakosi huduma katika kipindi hiki cha mpito.

Hivyo, endapo mwanachama atapata changamoto yoyote awasiliane na Mfuko kupitia Ofisi zake zilizoko nchi nzima pamoja na Kituo cha Huduma kwa Wateja kinachofanya kazi saa 24 kila siku kupitia namba 199 bila malipo.

Imetolewa na;

Grace Michael

KAIMU MENEJA UHUSIANO